# WeBUILD TANZANIA FOUNDATION (WBTF)

WeBUILD TZ-FOUNDATION

FOR BETTER TOMORROW

KUHUSU SISI

Dar es salaam

Simu: 0743 444 999

webuildtanzaniafoundation@gmail.com

https://webuildfoundation.co.tz/

Instagram@webuildtz

1. JINA LA ASASI
WeBUILD TANZANIA FOUNDATION (WBTF)

2. MAKAO MAKUU YA ASASI

Makao makuu ya Asasi yatakuwa mkoa wa Dar es salaam wilaya ya Ilala

3. ANUANI YA ASASI

P.O BOX 31324

Dar es salaam

## *Utangulizi*

Jamii nyingi nchini Tanzania, hasa kaya zenye kipato cha chini na makundi maalum (yatima, wajane, wazee, walemavu, wanawake wanaolea bila wenza, na wanafunzi wasiojiweza), zinakabiliwa na changamoto za kujitegemea kiuchumi. Watoto kutotambua haki na wajibu wao. Licha ya rasilimali zilizopo, kuna ukosefu wa ufahamu wa fursa za kiuchumi, kufikia wadau,elimu ya ujasiriamali, na ujuzi wa kuanzisha na kusimamia miradi. Desturi duni za kuweka akiba, elimu hafifu ya afya, miundombinu duni, na ukatili wa kijinsia. Kupungua kwa maadili na ufahamu wa urithi wa taifa kwa kizazi cha Gen Z kunadhoofisha mshikamano na utaifa. Shirika hili kwa kushirikiana na Serikali na wadau, linalenga kutoa msaada wa haraka na suluhisho za muda mrefu kupitia uwezeshaji wa kiuchumi,elimu, mafunzo ya ujuzi, miradi endelevu, na kuimarisha maadili ili kujenga jamii imara, inayojiamini yenye fursa sawa kwa wote.



# Dira

Jamii endelevu, jumuishi na yenye haki na usawa, ambapo hakuna anayeachwa nyuma kwa ajili ya kesho njema iliyo bora.

# Dhamira

Kuboresha maisha ya jamii zilizoachwa nyuma katika mazingira magumu kwa msaada wa haraka kupitia elimu, upatikanaji wa rasilimali, mafunzo ya ujuzi, kujali afya na ustawi binafsi (self-care), pamoja na kutoa fursa za kukuza uchumi na maendeleo ya jamii ya muda mrefu.



# Malengo

1. Kusaidia kaya maskini zenye hali ya chini katika jamii pamoja na makundi maalum.

2. Kukuza uwezeshaji wa kiuchumi, kujenga na kuimarisha maisha endelevu ya jamii, uwezeshaji binafsi, kuwafikia wadau, kuanzisha na kusimamia miradi itakayoongeza na kuboresha kipato kupitia ujasiriamali, kilimo, ufugaji n.k.

3. Kuimarisha uwezo, usimamizi wa kifedha na uhuru wa Kiuchumi, kukuza utamaduni na elimu ya kuweka akiba ili kufikia malengo na kutatua dharura.

4. Kujenga na kuchochea ukuaji wa maendeleo endelevu ya jamii ya muda mrefu kwa kufanya tathmini kupitia wasifu wa kijamii wa kiuchumi na programu zinazokuza ushiriki wa wananchi, upatikanaji fursa na utatuzi wa changamoto.

# Malengo

5. Kukuza utatuzi wa mogogoro na haki za kijinsia kwa njia ya amani, kupinga ukatili na kuhamasisha usawa.

6. Kuhakikisha upatikanaji kwa usawa wa huduma muhimu na miundombinu kwa makundi maalum.

7. Kukuza afya na kinga dhidi ya magomjwa kwa ustawi wa jamii, elimu

ya magonjwa kama sickle cell, wajawazito utumiaji wa folic acid kuepuka watoto kuzaliwa na vichwa vikubwa, magonjwa ya afya ya akili n.k.

8.Kuhifadhi asili na historia, kulinda, kuendeleza, Kukuza Utamaduni na urithi

wa Kitanzania.



# TUNATAZAMIA

1. Kuongeza elimu na ujuzi kwa jamii
2. Kukuza uwezeshaji wa kiuchumi na maisha endelevu
3. Kuwezesha upatikanaji wa rasilimali na huduma muhimu
4. Kujenga na kuimarisha uwezo wa jamii
5. Kuhifadhi na kuendeleza tamaduni na mila
6. Kukuza uwezeshaji binafsi na kujithamini
7. Kutoa msaada wa haraka kwa makundi yaliyo katika mazingira magumu
8. Kujenga maendeleo ya jamii ya muda mrefu

# MAMA INUKA TANZANIA

## “Tujenge Nguvu ya Mama, Tukuze Uchumi wa Jamii.”



Mradi wa Mama Inuka Tanzania ni mpango wa uwezeshaji wa kiuchumi unaolenga akina mama wajasiriamali wadogo katika mikoa ya Dar es Salaam, Tanga, Morogoro na Pwani. Mradi unalenga kuwafikia moja kwa moja katika maeneo yao ya biashara ili kutambua changamoto zao na kuwapa msaada wa kitaalamu na kimtaji., kwa kuwapatia mafunzo ya biashara, usimamizi wa fedha, uboreshaji wa bidhaa, pamoja na kuwaunganisha na fursa za mitaji na masoko.

# MTOTO SALAMA, TAIFA IMARA

Mradi wa Elimu na Ulinzi wa Haki za Mtoto

Lengo la Mradi

Kuhakikisha kila mtoto anapata:

- Elimu bora na salama
- Ulinzi dhidi ya ukatili na unyanyasaji
- Malezi yenye upendo na msaada
- Uelewa wa haki za mtoto

"Mtoto aliye salama leo, taifa imara kesho."

WeBUILD TZ-FOUNDATION
FOR BETTER TOMORROW

WeBUILD TANZANIA FOUNDATION

# Thank you

